# UJIRANI Mwema

HIFADHI NA JAMII

Julai-Septemba 2021



## COCOBA SERENGETI: MKOMBOZI WA MAENDELEO NA UHIFADHI

PAGE 6

## TUZO YA TANAPA NYANDA ZA JUU YAZIDI KUSHAMIRI

PAGE 8

## HIFADHI YA TAIFA ARUSHA INAVYOUNGA MKONO MIRADI YA WANANCHI

PAGE 11

**Bodi ya Uhariri**

Mhariri Mkuu:
Allan Hebert Kijazi

..............

Mhariri Mwandamizi:
William Simon Mwakilema

................

Wahariri Wasaidizi:
Godwell Ole Meingataki
Catherine Gerald Mbena
Samwel Nassari

...................

Wahariri Washauri:
Claud Gwandu
Deus Ngowi

...................

Wasanifu wa Kurasa:
Kitengo cha Uchapishaji - TANAPA




UJIRANI MWEMA ni jarada linalotolewa na Hifadhi za Taifa Tanzania Kitengo cha Uhifadhi Mahusiano ya Jamii, TANAPA Makao Makuu, Barabara ya Dodoma, S.L.P. 3134, Postikodi 23106 Arusha-Tanzania
Uchapishaji na kitengo cha uchapishaji TANAPA

# YALIYOMO

4
TAHARIRI

INAVYONUFAISHA EMANYATA KAKOI KWA NYUKI

6
COCOBA SERENGETI MKOMBOZI WA MAENDELEO NA HIFADHI

17
IBANDA-KYERWA NA RUMANYIKA KARAGWE: CHACHU YA UHIFADHI YAKUA

8
TUZO YA TANAPA NYANDA ZA JUU YAZIDI KUSHAMIRI

18
HIFADHI YA SAADANI NA MRADI WA USHIRIKIANO WA ZAHANATI YA MKANGE

11
INAVYOUNGA MKONO MIRADI YA WANANCHI

20
JITIHADA ZA KUNUSURU USHOROBA NA MFUMO WA IKOLOJIA GOMBE ZAANZA KUZAA MATUNDA

13
HIFADHI YA TARANGIRE









23
ULINZI SHIRIKISHI WAPUNGUZA UJANGILI WA SAMAKI RUBONDO

25
ELIMU YA UHIFADHI KUGAWANA FAIDA VYAPUNGUZA UJANGILI MIKUMI

28
MRADI MKUBWA WA UFUGAJI NYUKI KUWA NEEMA KWA WAVIU

32
USHIRIKISHWAJI WANANCHI WAMALIZA MIGOGORO YA MIPAKA MIKUMI










# TAHARIRII



**Msomaji mpendwa**

Mpango wa Ujirani Mwema katika Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ulianza kutekelezwa zaidi ya miaka 35 iliyopita, kwa lengo la kuhamasisha ushiriki wa jamii zinazopakana na hifadhi za taifa katika uhifadhi wa maliasili na mazingira. Kufikia azma hii, TANAPA imekuwa ikitekeleza shughuli mbalimbali zenye faida kwa jamii hizo.

Miongoni mwa shughuli hizo ni elimu ya uhifadhi yenye lengo la kuwajengea uelewa mzuri wanajamii hao kuhusu masuala mbalimbali ya uhifadhi, ikiwa ni pamoja na faida zake, mbinu za uhifadhi, umuhimu wa wanajamii wenyewe katika kuendeleza uhifadhi na kuboresha mahusiano baina ya Jamii na hifadhi.

TANAPA imeshirikiana kikamilifu na jamii na kuchangia utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo iliyoibuliwa na jamii husika kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa huduma bora  kwenye sekta mbalimbali hasa elimu, afya, maji, mipango ya matumizi bora ya Ardhi na usalama.

Mathalani, kwa kipindi cha miaka kumi (2010-2020), TANAPA iliwekeza zaidi ya shilingi bilioni 13 kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa miradi 327 katika vijiji jirani na hifadhi za taifa.

TANAPA imefanikiwa kuviwezesha vikundi mbalimbali vya ujasiriamali, miongoni mwa wanajamii, ili kutekeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi zisizo na madhara kwa mazingira, kama vile ufugaji wa nyuki na samaki, kilimo cha matunda na mboga mboga na ususi ili kuinua kipato cha kaya na kupunguza utegemezi kwenye rasilimali za asili. Kwa kipindi cha kuanzia 2015 hadi sasa, takribani shilingi bilioni moja zimetolewa kuwezesha vikundi 78 vya ujasiriamali katika jamii.

TANAPA imefanikiwa kuboresha mahusiano na jamii zinazopakana na hifadhi na hii inadhihirishwa na hamasa kubwa waliyonayo wanajamii ya kutoa taarifa za siri zinazosaidia ukamataji wa majangili pamoja na nyara za Serikali

Aidha, kwa jamii husika mbali na manufaa ya kimaendeleo waliyoyapata kwa kupitia michango ya moja kwa moja ya TANAPA, baadhi yao zimefaidika na shughuli za utalii zinazofanyika katika maeneo yao na ndani ya hifadhi kwa kujipatia ajira za muda mrefu na mfupi pamoja na kupata masoko kwa ajili ya bidhaa zao mbalimbali kama mazao ya shamba na mifugo, ususi, ufinyanzi na utamaduni.

Hata hivyo, zipo changamoto kadhaa ambazo zinaukabili mpango huu wa Ujirani Mwema ambazo ni pamoja na ufinyu wa rasilimali fedha hasa kutokana na kuongezeka kwa hamasa miongoni mwa wanajamii na ongezeko la idadi ya vijiji lengwa katika maeneo jirani na hifadhi, hasa baada ya kuanzishwa kwa hifadhi za Taifa mpya.

Changamoto nyingine ni pamoja  na ongezeko la shughuli za binadamu katika maeneo yanayopakana na Hifadhi baada ya wageni kuhamia kutokana na fursa za kiuchumi zinazofunguka katika maeneo hayo. Hii ni pamoja na ulishaji mifugo ndani ya maeneo ya hifadhi, mioto kichaa, wanyamapori waharibifu na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa ufupi, kwa ushirikiano wa pamoja, tumepata mafanikio mengi na makubwa katika utekelezaji wa Mpango wa Ujirani Mwema kati ya Shirika la TANAPA na jamii husika ambayo yamewaletea maendeleo wananchi lengwa sambamba na kuboresha mahusiano baina na wananchi  na hifadhi wanazopakana nazo Hata hivyo, Shirika limejipanga kuwekeza katika kuhamasisha ushiriki wa wadau mbalimbali katika kutekeleza Mpango huu wa Ujirani Mwema, ikiwa ni pamoja na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali.

**Karibuni Sana.**



..................................

**Dk. Allan H. Kijazi**

# Ujumbe kutoka kwa mhariri



Tunayo furaha kukualika katika Jarida letu upate nafasi ya kusoma na kupitia taarifa na habari motomoto zinazohusu masuala ya ujirani mwema kutoka katika Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

Jarida letu la Ujirani Mwema linaandaliwa na Kitengo cha Mahusiano ya Jamii cha TANAPA, na litatoka kila baada ya miezi mitatu.

Jarida hili litaendelea kutoa fursa kwa wahifadhi na wadau wetu kupata habari zinazotoka uwandani kuhusiana na jitihada za TANAPA katika kutekeleza shughuli za uhifadhi kwa kuwashirikisha wananchi na wadau wengine pamoja na kuonyesha kwa vitendo mchango na faida ya uhifadhi kwa jamii na Taifa.

Kupitia makala mbalimbali, jarida letu litabainisha jinsi TANAPA inavyotumia mbinu na mikakati mbalimbali kujenga mahusiano na jamii, kuwashirikisha wananchi katika shughuli za uhifadhi, kutoa Elimu ya Uhifadhi, kuandaa mipango endelevu ya matumizi bora ya Ardhi, kutekeleza miradi ya kijamii, miradi ya kuongeza kipato kwa wananchi kupitia vikundi vya kijamii hivyo kuleta manufaa kwa mtu mmoja mmoja

Toleo hili lina makala mbalimbali ambazo zinaonyesha jitihada za kujenga na kuimairisha ujirani mwema na ushirikiano na jamii zinazoishi karibu na hifadhi. Kwa ujumla, TANAPA ina hazina kubwa na uzoefu katika kushirikisha jamii, hivyo kupitia makala mbalimbali katika jarida hili tutaendelea kuelezea na kuonyesha yale ambayo Shirika linafanya katika kuendeleza uhifadhi na kuchangia katika maendeleo ya jamii.

Ni mategemeo yetu kuwa wasomaji wa jarida hili watafurahia na kujifunza mengi. Tutafurahi kupokea maoni, ushauri na mapendekezo ili kuboresha jarida hili.

**“Uhifadhi endelevu, kwa maendeleo”**

# COCOBA SERENGETI:

## MKOMBOZI WA MAENDELEO NA UHIFADHI



### Mkombozi wa maendeleo na uhifadhi

***Na Hobokela Mwamjengwa,***

“ Nimepata maendeleo makubwa tangu nilipojiunga na kikundi cha Cocoba Tuleane miaka mitatu iliyopita. Nimejenga kibanda, nina biashara yangu,nafuga mbuzi, kondoo na kuku.

“Ninasomesha watoto wangu na, kwa kweli hali yangu inaridhisha,ninajitegemea na ninaisaidia familia yangu,”anatoa ushuhuda Dotto Bukindu mkazi wa kijiji cha Bukore wilayani Bunda na mama wa watoto watatu na mwamachama wa kikundi cha COCOBA Tuleane,moja ya vikundi vilivyoanzishwa kwa msaada wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Ushuhuda wa Dotto unatokana na vikundi vilivyoanzishwa ili kuwasaidia wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hiyo kuwa na miradi ya kiuchumi na kuusaidia katika shughuli za uhifadhi na utunzaji wa mazingira

Kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, Hifadhi hiyo maarufu duniani imetumia zaidi ya sh milioni 243 kwa ajili ya kujenga uwezo wa wananchi katika kuanzisha, kusimamia na kuendeleza vikundi vya COCOBA.

COCOBA ni kifupi cha maneno ya kiingereza “Community Conservation Bank” ikamaanisha Benki Hifadhi ya Jamii. COCOBA ni mfumo wa kibenki unaotumika vijijini ambao huwawezesha wananchi kutengeneza mitaji kwa njia ya kuweka akiba na kununua hisa ili kupata huduma ya mikopo midogo-midogo yenye riba nafuu na kwa urahisi. COCOBA huendeshwa kwa njia ya vikundi ambapo mwanachama baada ya kuweka akiba anaweza kupata mkopo mara mbili au tatu kulingana na akiba aliyoweka.

Mikopo hiyo imekuwa msaada kwa wanachama kwa kuinua kipato chao na kuboresha shughuli za uzalishaji. Kwa kuwa COCOBA ni benki ya kijamii inayohusisha uhifadhi, mikopo inayotolewa ni ile ambayo inalenga kutekeleza miradi inayosaidia utunzaji wa mazingira na uhifadhi.

Emanuel Robert Mashauri (41),mkazi wa kijiji cha Salalia kilichopo wilaya ya Bariadi ni mmoja wa wanufaika wa kikundi cha COCOBA ambacho alijiunga miaka mitatu iliyopita.

“Kabla ya kujiunga nilikuwa sijui namna ya kuweka akiba,kutunza kumbukumbu za mapato yangu, lakini sasa najivunia kuwa mwanakikundi na kwa kweli tunaishukuru sana SENAPA (Serengeti National Park) kwa kutusaiia kuanzisha vikundi hivi ambavyo ni mkombozi wetu kiuchumi”

Anaongeza kuwa kabla ya kuingia rasmi kwenye kikundi walipewa mafunzo ya namna ya kuweka akiba na baadaye kutumia akiba hiyo kama mtaji wa kufanyia mambo mengine ya kiuchumi kwa kukopa na urejeshaji wa mkopo kitu ambacho hawakuwa wakiktambua hapo awali.

“Ninaweza kuendesha biashara zangu kutokana na mkopo nilioupata kutoka kwenye kikundi chetu na sasa nasomesha watoto wangu bila kubabaika kwa sababu nina kipato cha uhakika,” anasisitiza Mashauri,baba wa watoto wanne.



Kweli COCOBA ni mfumo wa kipekee kwa sababu hutoa fursa kwa wananchi kujenga tabia ya kuweka akiba na kukopa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuhamasisha uhifadhi na utunzaji wa mazingira. Taasisi mbalimbali za uhifadhi zimekuwa zikitumia mfumo wa COCOBA kama chombo cha kufikia malengo ya uhifadhi na ustawi wa jamii ziishizo pembezoni mwa maeneo ya Hifadhi. COCOBA imekuwa kiunganishi kati ya uhifadhi wa maliasili na ustawi wa jamii. Wanachama katika vikundi hivyo wamejiwekea miiko ya kutofanya biashara ya nyama itokanayo na wanyamapori na kutochoma au kujishughulisha na biashara ya kuuza mkaa.

Mhifadhi wa Ujirani Mwema katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Hobokela Mwamjengwa anasema kuwa katika kipindi cha mwaka 2018 – 2019 Hifadhi hiyo imewajengea uwezo wananchi kuanzisha na kusimamia vikundi vya COCOBA kwenye vijiji 10 vinavyopakana na Hifadhi katika Wilaya za Bunda na Bariadi. Vijiji vilivyonufaika na mpango huo ni Tingirima, Kyandege, Mugeta, Mariwanda, Kihumbu, Hunyari na Bukore katika wilaya ya Bunda na katika wilaya ya Bariadi ni; Mwantimba, Matongo na Salalia. Jumla ya vikundi 16 vya COCOBA vimenzishwa katika vijiji hivyo ambapo Hifadhi imewezesha mafunzo ya kujenga uwezo wa kuanzisha, kusimamia na kuendesha COCOBA, vilevile vimepatiwa mafunzo ya uanzishaji na usimamizi wa miradi/ biashara, ujasiriamali, uandishi wa taarifa za fedha, utunzaji wa kumbukumbu, utengenezaji wa katiba, usimamizi wa fedha na upangaji na usimamizi wa miradi.

Anasema tangu kuanzishwa kwa vikundi hivyo mwaka 2018 vimeweza kutengeneza mtaji wa sh 121,138,900 na kutoa mikopo yenye thamani ya sh 102,146,600

Aidha vikundi 8 vya COCOBA katika Wilaya ya Bariadi vimepatiwa jumla ya mizinga ya nyuki 160, ambapo kila kikundi kilipata mizinga 20 kwa ajili ya kuanzisha mradi wa kufuga nyuki. Vikundi hivyo pia vimepatiwa mashine ya kufyatua tofali za kujengea majiko banifu na pikipiki ili kurahisisha usimamizi wa miradi ya vikundi na uendelevu wa vikundi hivyo.

Sambamba na kupatiwa vifaa hivyo vikundi hivyo vimepatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki, ufugaji kuku, ufugaji wa samaki na kilimo cha mbogamboga na matunda kwa ajili ya kuanzisha miradi itakayoendana na mafunzo hayo.

Vilevile wanachama 173 kati ya 214 wa vikundi hivyo wamewezeshwa kujengewa majiko banifu ambapo kila mwanachama alijengewa jiko moja.

“ Wanachama wa COCOBA wanatarajiwa kuwa mawakala wa uhifadhi kwa kuhamasisha uhifadhi na utunzaji wa maliasili na mazingira kwa jamii inayowazunguka,”anasisitiza Mwamjengwa.



Kwenye picha wanachama wa COCOBA wakishiriki maonesho ya nanenane

# TUZO YA TANAPA YAIMARISHA MAZINGIRA NYANDA ZA JUU KUSINI

Tuzo mbalimbali Uhifadhi Mazingira Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. (TANAPA-CEAS) zikitolewa kwenye vikundi katika Halmashauri tano za wilaya ambazo ni Kilolo na Mufindi mkoani Iringa, Mbarali iliyoko mkoani Mbeya na Wanging'ombe na Makete ambazo zipo mkoani Njombe

## Kiasi cha sh. Milioni 90 kimetumika kuwapa zawadi washindi katika makundi mbalimbali yaliyoshinda kwa kipindi cha miaka 4.

***Na Yassin Sharif,***

UCHAFUZI wa mazingira na matumizi yasiyo endelevu ya maliasili ni moja ya changamoto kubwa zinazodumaza dhana nzima ya maendeleo katika nchi nyingi zinazoendelea ikiwemo Tanzania. Uendelezaji wa shughuli za kibinadamu ndani na kandokando mwa vyanzo vya maji, hususani ukataji holela wa miti kwa ajili ya matumizi ya mkaa kuni na ujenzi, kilimo, utupaji wa taka ngumu maeneo yasiyo rasmi, ufugaji na ulishaji wa mifugo usiokuwa na tija ni miongoni mwa sababu zinazo sababisha kukauka kwa vyanzo vingi vya maji.

Kuendelea kwa shughuli zisizo rafiki na mazingira kunachangia milipuko




ya magonjwa mbalimbali kama vile ya kuhara lakini pia ukame wa muda mrefu kutokana na unyeshaji wa mvua usiotabirika unaosababishwa na mabadiliko ya Tabianchi. Unyeshaji wa mvua usiotabirika husababisha kukosekana kwa mapato ya uhakika kutokana na kushuka kwa uzalishaji katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, utalii na viwanda na hivyo kuchangia kudorora kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla

Shughuli za kilimo kandokando ya vyanzo vya maji husababisha kutokea kwa mmomonyoko wa udongo ambao nao husababisha mchanga kujaa kwenye mito na hivyo mito kupoteza mikondo yake na mingine kukauka.

Migogoro mingi inayojitokeza mara kwa mara baina ya Jamii (Wafugaji, Wakulima, Wavuvi) na Wahifadhi katika maeneo yaliyotengwa na kuhifadhiwa kama Hifadhi za Taifa, ni kutokana na kukosekana kwa mpango mkakati wa matumizi bora ya ardhi, huduma muhimu za kijamii kama vile mahitaji ya maji safi na salama, chakula, malisho ya mifugo ambavyo vyote husababishwa na uharibifu wa mazingira.

**Tuzo ya TANAPA ya Kuhifadhi Mazingira**

Katika kukabiliana na changamoto ya uchafuzi wa mazingira, vyanzo vya maji na uhifadhi wa Ikolojia ya Mto Ruaha Mkuu, Mwaka 2015/16 Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kupitia Hifadhi za Taifa za Ruaha, Kitulo na Milima ya Udzungwa ilianzisha Tuzo ya Uhifadhi Mazingira Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. (TANAPA-CEAS) inayoshirikisha Halmashauri tano za wilaya ambazo ni Kilolo na Mufindi mkoani Iringa, Mbarali iliyoko mkoani Mbeya na Wanging'ombe na Makete ambazo zipo mkoani Njombe

Mratibu wa Tuzo hiyo,Yassin Sharif anasema kuwa katika kufanikisha utoaji wa tuzo hiyo wadau mbalimbali walishirikishwa ikiwa ni pamoja na Mradi wa Mtandao wa Maeneo ya Hifadhi Kusini mwa Tanzania (SPANEST), Bodi ya Maji Bonde la Rufiji, Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Wanyamapori (WWF) , Taasisi ya Kimataifa ya Kijamii ya Uhifadhi wa Wanyamapori (WCS).




Anasema kuwa tuzo hiyo inatolewa kwa washindi watatu kutoka kila Wilaya ambapo huadhimishwa kila mwaka katika Wiki ya Mazingira Juni 5. Tangu kuanzishwa kwa tuzo hiyo imeonekana kuwa na mapokeo mazuri kutokana na kufungua fursa nyingi za uwekezaji ambazo awali hazikuweza kuonekana moja kwa moja, jambo ambalo liliwapa ugumu wanajamii kutoa ushirikiano juu ya masuala ya uhifadhi wa mazingira, na hasa vyanzo vya maji (mito) na misitu.

**Malengo:** Kwa mujibu wa mratibu huyo, tuzo ya uhifadhi mazingira inalenga kuokoa, kulinda na kuinua maslahi na uchumi wa mtu mmoja mmoja, kanda na taifa kwa ujumla. Kuokoa mfumo wja ikolojia katika maeneo ya hifadhi hususan ya Ruaha, Kitulo na Milima ya Udzungwa kwa kushirikisha mwana jamii moja kwa moja katika masuala ya uhifadhi wa mazingira ili kuokoa maliasili za nchi lakini kunusuru vyanzo vya maji katika Wilaya ya Makete ambapo vyanzo vya maji 966, Mbarali 32, Wanging'ombe 510, Kilolo 25 kati ya 1,021 na Mufindi 151 kati ya 1,700 vimeainishwa na kusimamiwa.

Makundi ya Washiriki wa tuzo wanatoka katika wilaya hizo tano wakiwemo watu binafsi, Serikali za vijiji, taasisi mbalimbali kama vile shule za msingi na Sekondari, Jumuiya za watumia maji na Hifadhi za Wanyamapori za Jamii (WMA)

**Makundi ya kushindania ni kama ifuatavyo:** Vitu vinavyozingatiwa kwenye shindano hilo ni pamoja na uhamasishaji na utoaji elimu ya mazingira, uhifadhi wa vyanzo vya maji (kingo za mito, chemchemi), upandaji miti ya asili, uhifadhi wa misitu ya asili, uhifadhi wa ardhi oevu, uhifadhi wa mifumo ya Ikolojia yaani shoroba na hifadhi za wanyamapori za Mtawanyiko.

Awali TANAPA ilikuwa na programu ya kuelimisha jamii zinazoishi jirani na hifadhi juu ya masuala ya kutunza, kuhifadhi na kulinda maliasili na mazingira kwa kuanzisha bustani za miti asili, kuwezesha vikundi vya ufugaji nyuki, elimu ya uhifadhi katika shule na vijiji katika maeneo yanayozunguka hifadhi husika.

Programu hii ya Tuzo ya mazingiza imeleta matokeo chanya kwa kuweza kufikia jamii zilizopo mbali na hifadhi za taifa, lakini pia zenye athari katika mifumo ya ikolojia za hifadhi katika hifadhi hizi tatu.

**Matokeo ya Utekelezaji:** Tuzo ya mazingira ya TANAPA imefungua fursa za uwekezaji kwa jamii na hasa katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na maeneo ya jirani katika rasilimali za misitu, maji na hifadhi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, washiriki wa tuzo ya mazingira uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa mwaka 2017 toka Wanging'ombe walisema sababu kubwa iliyosababisha wengi wao kujiunga katika masuala ya uhifadhi wa mazingira ni kutokana na kukumbwa na adha ya kukosa maji katika maeneo wanayoishi, kukauka kwa vyanzo vya maji kunakosababishwa na kilimo cha bustani kwenye mabonde (kilimo cha vinyungu) kando kando na ndani ya vyanzo vya maji.

Mshindi wa kwanza toka wilaya ya Mbarali, Ambokile Mwanjisi anaeleza kuwa tuzo hii imewafungulia fursa na wameweza kujua namna bora ya kutumia maji na misitu katika kujiinua kiuchumi kwa kuwekeza kwenye ufugaji wa samaki, uanzishaji wa bustani za miti kwa ajili ya kuendeleza misitu yao lakini pia kufanya biashara ya uuzaji wa miche ya miti.

" Vilevile tunafuga nyuki kwenye misitu yetu ambao pia wanatumika kama walinzi, lakini pia tunapata kipato kutokana na kuvuna asali na mazao mengine ya nyuki,"anasisitiza Mwanjisi.

Tuzo hiyo imeongeza kasi na muda wa mtiririko wa maji katika Mto Ruaha Mkuu ili kunusuru wanyamapori wanaopatikana katika Hifadhi ya Ruaha, kurejesha uoto wa asili na ongezeko la wanyama katika bonde ya Ihefu. Uhakika wa upatikanaji wa maji ya kuzalisha nishati ya umeme katika Bwawa la Mtera na Bwawa la Mwalimu Nyerere wa ajili ya uendeshaji wa viwanda, ukuzaji wa uchumi wa taifa na matumizi ya majumbani. Pia kuiendeleza sekta ya utalii na hasa katika kuilinda na kuitangaza Hifadhi ya Taifa Ruaha ambayo ni ya pili kwa ukubwa nchini na ya tatu kwa ukubwa barani Afrika.

Mratibu wa Tuzo wa Wilaya ya Mbarali, Patrick Charles, ameelezea kuwa Tuzo hiyo imekuwa nyenzo muhimu na ya kipekee katika kuhamasisha wanajamii kushiriki katika masuala ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira katika maeneo yanayowazunguka. Anaongeza: " Tuzo imeongeza ari na hamasa kwa Jamii katika kushiriki uhifadhi wa vyanzo vya maji, misitu, ardhi, wanyamapori na mazingira kwa ujumla katika maeneo mengi ambako Jamii imeelimishwa na inazingatia elimu hiyo ya uhifadhi wa mazingira.

" Kipato kinachopatikana kimesaidia baadhi ya wanajamii husika, walioshiriki na kushinda, kuanzisha miradi midogo ya uzalishaji mali ambayo ni rafiki wa mazingira"

Toka Mwaka 2016 hadi 2020 jumla ya washindi 80 kwa wilaya zote tano kila wilaya ikiwa na washindi 3 kila mwaka wamepatikana.

Kiasi cha sh. Milioni 90 kimetumika kuwapa zawadi washindi katika makundi mbalimbali yaliyoshinda kwa kipindi cha miaka 4. Toka tuzo hii kuanza kumekuwa na ongezeko la washiriki kadri uhamashishaji unavyoendelea. Katika mwaka 2016, jumla ya washiriki 56 walishiriki tuzo hizi na kwa mwaka 2020 washiriki walifikia 395 katika makundi mbalimbali.

Ongezeko la washiriki wa kuwania tuzo hiyo kunatoa nafasi kwa wataalamu wa masuala ya mazingira na hasa wanaokuwepo katika Kamati za Tathmini za Miradi iliyoingia katika shindano kutoa elimu, kuhamasisha lakini pia kutambua changamoto mbalimbali ambazo jamii na vikundi vya mazingira wanakumbana nazo na kuwashauri namna nzuri ya kukabiliana nazo. Kamati ya Mazingira ya TANAPA inatoa nafasi kwa washiriki kujadiliana moja kwa moja na wataalamu wa masuala ya mazingira kuhusiana na utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Katika kuadhimisha siku ya mazingira duniani iliyofanyika katika Kijiji cha Matamba mwaka 2019, Wakuu wa mikoa na Wilaya akiwemo, mgeni zasmi Mhe. Christopher Ole Sendeka (Njombe) walionyesha wazi kufurahishwa na mpango mkakati na kuipa pongezi TANAPA kwa kuanzisha tuzo hizo kwa kushirikisha jamii.

Pia wakuu hao wa mikoa wamekuwa wakiwataka viongozi wa serikali kuanzia vijiji, kata na wilaya na wananchi kwa ujumla kuhakikisha wanasimamia suala la utunzaji wa mazingira kuanzia ngazi ya familia kwa kuanza na upandaji wa miti ili kufikia malengo ya wilaya, mkoa na hatimaye taifa.

Kuandaa na kusimamia matumizi bora ya ardhi katika vijiji, kuwa na matumizi endelevu ya maliasili, kufanya kilimo chenye tija ni utekelezaji wa sera ya Tanzania ya viwanda kwa kuzalisha malighafi zenye ubora kwa kufuata kanuni za kilimo cha kisasa.

# HIFADHI YA TAIFA ARUSHA INAVYOUNGA MKONO MIRADI YA WANANCHI



Kazi liyofanywa na ANAPA ni ujenzi wa madarasa mawili na ofisi ya walimu Shule ya Sekondari Losinoni, ujenzi wa madarasa mawili, ofisi ya walimu na ununuzi wa samani (madawati 90, meza mbili na viti vinne vya ofisi ya walimu) katika Shule ya Sekondari Ngurdoto.

Na Mary Mtenga,

WANANCHI wanaoishi karibu na Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ni wadau muhimu katika maendeleo ya uhifadhi na utalii nchini.

Kwa maana hiyo unatakiwa ushirikiano baina ya Hifadhi na wananchi ili kwanza kuhakikisha uboreshaji wa uhifadhi wa mazingira, Wanyamapoli na hali za wanajamii kiuchumi na kijamii unafikiwa.

Idara ya Mahusiano ya Jamii katika Hifadhi ya Taifa Arusha (ANAPA) imeweka utaratibu wa kuunga mkono jitihada za wananchi kwa kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo, sambamba na utoaji wa elimu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2015/2016 hadi 2019/2020, Hifadhi, kwa kushirikiana na wananchi wa vijiji vya Oldonyowas, Losinoni, Olkungw`ado, Nkoasiyo, Nkoanekoli na Ngurdoto, imefanikiwa kujenga madarasa ya shule na ofisi za walimu, nyumba za walimu na ununuzi wa samani kwenye shule za sekondari na msingi zilizopo katika vijiji hivyo.

Miradi hii ya Ujirani Mwema iliyotekelezwa na Hifadhi katika kipindi hicho ni pamoja na Ujenzi wa madarasa mawili, ofisi ya walimu na ununuzi wa samani (madawati 90, meza mbili na viti vinne vya ofisi ya walimu) katika Shule ya Sekondari Oldonyowas,

Mkuu wa Shule ya Sekondari Oldonyowas, Richard Mugyabuso anatoa shukurani kwa ANAPA na TANAPA, akisema wamebadilisha kabisa mandhari ya shule yake, wakiiweka juu sana kihadhi kwa miundombinu na samani.

Anakwenda mbali zaidi na kusema kuna baadhi ya viongozi wa maeneo mengine wakiiona ofisi ya mkuu wa shule hiyo wangetamani iwe yao kwa jinsi ilivyojengwa vyema na kwa kiwango cha juu sana.

"ANAPA wametujali na kutupatia makubwa katika madarasa, samani kama madawati 90, lakini pia ofisi nzuri. Hawa wamekuwa tofauti na watoaji wengine, kwa sababu vitu walivyotupa vinadumu na viwango vyake ni vya hali ya juu," anasema Mugyabuso akijawa Furaha.

"ANAPA ndio waliosaidia shule kufunguliwa 2017/18, ina maana kwamba bila ufadhili wao shule haingekuwapo. Kwa hiyo shule imeanza na inasonga mbele vizuri katika mazingira bora," anasema Mugyabuso.

Wanafunzi nao wanatoa shukurani kwa ANAPA na TANAPA. Heavenlight Godfrey ni mwanafunzi wa kidato cha tatu anayesema msaada wa ANAPA kwa shule yao ni mkubwa, akisema



anajua walisaidia ujenzi na kutoa meza, viti na kadhalika, ambapo awali walikuwa katika mazingira magumu.

"Awali hatukuwa na viti wala meza; tulikuwa tukipata shida na wakati mwingine tulikuwa tukiazima kwenye shule ya msingi lakini sasa tunasoma na kujifunza kwa utulivu na raha kwa sababu ANAPA wametujal. Tunapta elimu bora na tutajitahidi zaidi, tunawashukuru," anasema Godfrey.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Oldonyowasi, Geoffrey Samson Ayo anasema wamefaidika vikubwa na mchango wa ANAPA kwao na kwa kufanya hivyo wameonesha mshikamano na wao kwa kurudisha ni kuhifadhi mazingira na kuhakikisha utalii unakua.

Kama ilivyo kanuni za TANAPA - kwa hifadhi husika kuchangia asilimia 70 na wananchi wa vijiji vinavyozunguka hifadhi kuchangia asilimia 30, wananchi walishiriki katika kusomba mchanga, mawe, maji na kuweka nguvukazi.

Ayo anasema kwamba tangu mwanzo walishiriki kama jamii, wakaweka jamvi kwenye msingi wa majengo na ANAPA wakaja kupandisha kuta, kumalizia ujenzi na pia kuweka samani.

Ama kuhusu uhifadhi, Ayo anasema Oldonyowasi ni kijiji cha mfano, kwa sababu wamekuwa wakipambana kuhakikisha hakuna mioto inayotokea ndani wala jirani na hifadhi na wamekuwa wakifanya operesheni kuhakikisha hakuna kuingiza mifugo wala watu kufanya kilimo kwenye hifadhi hiyo.

"Hii ni hifadhi yetu, ANAPA wanajua kwamba nasi ni watu wao kwa hiyo tuna ushirikiano mkubwa. Wanatusaidia kwenye miradi na sisi tunashiriki katika uhifadhi ili kukuza utalii na mapato. Tunazuia uwashaji moto, uvamizi wa aina yoyote, hakuna kuua Wanyama na kuona kwamba misitu inatunzwa," anasema Mwenyekiti Ayo.

Kazi nyingine iliyofanywa na ANAPA ni ujenzi wa madarasa mawili na ofisi ya walimu Shule ya Sekondari Losinoni, ujenzi wa madarasa mawili, ofisi ya walimu na ununuzi wa samani (madawati 90, meza mbili na viti vinne vya ofisi ya walimu) katika Shule ya Sekondari Ngurdoto.

Kadhalika, ANAPA imefanya ujenzi wa madarasa matatu katika Shule ya Msingi Olkung`wado, ujenzi wa nyumba pacha mbili za walimu katika shule za Sekondari Muungano-King`ori na Nkoanekoli zilizopo Wilayani Arumeru.

Jumla ya 281,341,592/- zilitumika kwenye miradi hiyo kama sehemu ya mchango wa Hifadhi wa asilimia sabini ambao ulitolewa wakati wa utekelezaji miradi ya Ujirani Mwema.

Kupitia miradi hii ya Ujirani Mwema, Jamii za vijiji jirani na Hifadhi kwenye vijiji vitatu vya Oldonyowas, Losinoni Juu na Ngurdoto zimefanikiwa kuanzisha shule za sekondari za kata pamoja na kuboresha mazingira ya kujifunzia wanafunzi na nyumba za kuishi walimu.

Miradi ya Ujirani Mwema inayotekelezwa na Hifadhi imekuwa na mchango mkubwa katika kuwapatia wananchi faida za kiuchumi na kijamii zinazotokana na shughuli ya utalii inayofanywa na Hifadhi. Hivyo mahusiano baina ya Hifadhi na Jamii za vijiji jirani yameimarika hali inayopelekea wananchi kuweza kushiriki kikamilifu katika shughuli ya ulinzi wa maliasili ndani na nje ya Hifadhi.

Idara ya Mahusiano ya jamii imefanikiwa kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi kwenye vijiji vya Oldonyowas, Losinoni Juu na Ngurdoto kutokana na uwepo wa miradi mbalimbali ya kijamii. Vikundi hivi vinasaidiana kwa karibu sana na Hifadhi, na kwa kiasi kikubwa vimetoa mchango wake katika kudhibiti uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za binadamu zinazokatazwa kisheria zikiwemo kilimo, mifugo, ukataji miti na uwindaji haramu wa wanyamapori.

Kwa pamoja tushiriki kikamilifu katika kuhifadhi mazingira na wanyamapori wetu ili tupate faida za kiuchumi, kijamii na kiikolojia.



# HIFADHI YA TARANGIRE INAVYONUFAISHA EMANYATA KAKOI KWA NYUKI

"Tunafurahi kwamba wananchi wamepokea vyema mradi huu na tunashirikiana nao na kuwasaidia kutatua changamoto". anasema Kamishna mwandamizi wa Uhifadhi Hifadhi ya Taifa Tarangire, Ignas Gara.



**Heriel Masaki,**

KIKUNDI cha Ufugaji Nyuki Emanyata kilichopo kijiji cha Kakoi, Wilaya ya Babati ni miongoni mwa vikundi vitatu vilivyowezeshwa na Hifadhi ya Taifa Tarangire.

Kikundi hicho cha Emanyata ambacho ni cha ufugaji wa nyuki kikiwa na washiriki 15, mchanganyiko wa wanawake na wanaume walipatiwa mafunzo pamoja na mizinga 45 na Hifadhi ya Taifa Tarangire kwa ajili ya ufugaji nyuki 2017.

Kwa kuwa kikundi hiki kinapatikana kwenye ukanda wenye miti aina ya migunga, wanakikundi waliamua kutumia fursa ya kufuga nyuki ambao hukusanya asali kutoka kwenye maua ya miti aina ya migunga ambayo ipo kijijini kwao na mingine ikipatikana kwenye Hifadhi.

Kikundi hiki kiliamua kujihusha na ufugaji wa nyuki kama fursa ya kuondokana na changamoto ya kukabiliana na wanyama waharibifu, hasa tembo katika mashamba yao yaliyo karibu na hifadhi.

Ezekiel Naibala ni Mweka Hazina wa Kikundi cha Emanyata Kakoi katika kitongoji cha Kigongoni, kilichoanzishwa 2016 na Shirika la Hifadhi Tanzania (TANAPA) kupitia Hifadhi ya Taifa Tarangire waliwafadhili mizinga ya kufugia nyuki.

"Tuliibua mradi huu wa kufuga nyuki mwaka 2016, tukaanza na mizinga sita ya kienyeji kisha tukaja na ya kisasa kwa kupewa na Hifadhi ya Taifa Tarangire mizinga 40 na yetu mingine 35 na pia Halmashauri ya Wilaya ikatupatia mzinga mmoja," anasema Naibala.

Kama kundi, Mwenyekiti Naibala anasema, tayari wameanza kuonja matunda ya uwekezaji huo unaohusisha pia uhifadhi na ukuzaji utalii, kwani kila wakivuna na kuuza hugawana asilimia fulani ya mapato kwa kila mwanachama.

Mwaka jana, kwa mfano, waligawana asilimia 35 ya mapato. Pamoja na mafanikio hayo, kuna changamoto kadhaa zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, kwani ukosefu wa mvua hupelekea mimea, ikiwamo miti, kutostawi na kutotoa maua yanayohitajika kwa nyuki. Wanalenga kwamba mwaka huu wapate lita 200 za asali na wanaweka sawa mtandao wa masoko ili kukidhi na kufaidika nao.

"Tunawashukuru na kuwapongeza sana wenzetu wa Hifadhi ya Taifa Tarangire na TANAPA kwa ujumla kwa ushirikiano na



Kikundi cha Ufugaji Nyuki Emanyata kilichopo kijiji cha Kakoi, Wilaya ya Babati ni miongoni mwa vikundi vitatu vilivyowezeshwa na Hifadhi ya Taifa Tarangire.

msaada wao, lakini pia sina budi kuwashukuru wana kikundi kwa ukubali na utayari wao kuwa pamoja kwenye kazi hii na uhifadhi," anasema mwenyekiti huyo.

Mbali na mambo ya ufugaji nyuki, wana Kamati ya Mazingira ya Kijiji inayoshirikiana na wana mgambo kwa ajili ya kudhibiti uharibifu wa mazingira. Kwa kawaida, mtu akikutwa na kosa la kwanza ambalo si kubwa hupewa onyo na akirudi hatua za kisheria hufuata mkondo wake, ukiwapo utaratibu wa kufikishwa mahakamani.

Wana kikundi wametumia fursa vizuri, kwa kuwa mizinga waliyopewa imekuwa chanzo cha mapato, sehemu ya dawa tiba, chakula pamoja na kukinga wanyama aina ya tembo kuharibu mashamba yao yaliyopo eneo lenye mizinga. Mbali na hayo, msitu wa kijiji eneo walikofugia nyuki leo limekuwa ni eneo zuri la msitu usioharibiwa na binadamu wala wanyama kama tembo kwa kuogopa ukali wa nyuki.

Mwezi Juni 2020 kikundi hiki kilifanikiwa kuvuna asali yao kwenye mizinga 24 kati ya 45 waliyo nayo na kujipatia zaidi ya lita 90 za asali iliyochujwa. Hii ni asali ya maua ya mgunga yenye sehemu kubwa ya tiba, kwani kwa karne kadhaa Wamasai wamekuwa wakitumia dawa za asili kutokana na miti hiyo ya migunga.



"Tunafurahi kwamba wananchi wamepokea vyema mradi huu na tunashirikiana nao na kuwasaidia kutatua changamoto. Hii ni nchi ya Savana yenye migunga mingi – maua mengi. Nyuki wapo wengi pia kiasi kwamba hata katika baadhi ya paa za majengo wapo hivyo bado kuna mahitaji zaidi ya makazi ya nyuki kwa maana ya mizinga. Kila mwaka tutaendelea kuomba fedha ili kuongeza ufadhili kwa vikundi," anasema Gara.

Kwa kuwa sasa wapo wilayani Babati kwa maana ya uwekezaji, Hifadhi ya Taifa Tarangire wanalenga kusogea kwa vikundi vingine wilayani Simanjiro, Monduli na ikiwezekana Kondoa.

Kutokoana na ubora wake, sehemu kubwa ya asali hii imeuzwa na wanakijiji na kununuliwa na watumishi wa hifadhi pamoja na wageni mbalimbali waliotembelea hifadhi. Jitihada zinazidi kufanyika na wanakikundi kupitia mafunzo waliopatiwa ili kuongeza mavuno zaidi na kuongeza ubora wa asali yao kwani mahitaji ya bidhaa hiyo yameonekana kuwa makubwa. Kwa kuwa wao ni wahifadhi wa siku nyingi wanasema wamelewa kuwa hii itakuwa njia nzuri ya kuhifadhi wanyama na mimea pasipo kileta athari kwa pande zote mbili.

Kamishna mwandamizi wa Uhifadhi Hifadhi ya Taifa Tarangire, Ignas gara, anasema kwamba wamejikita kusimamia uhifadhi na wanaona ufugaji nyuki kwa vijiji vinavyoizunguka hifadhi ni fursa nzuri, kwani asali huleta kipato – kukuza uchumi lakini pia ni kirutubisho kwa afya.

# IBANDA-KYERWA NA RUMANYIKA-KARAGWE: UHIFADHI WAKUA



Mzee Peter Akisoma shairi lake katika warsha

Wazee maarufu wawa mstari wa mbele kuhamasisha utalii, uhifadhi

**Fadhili Iddi,**

HIFADHI za Taifa Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe zilianzishwa Julai 05, 2019 kwa matangazo ya serikali (GN) na 509 na 510 mtawalia.

Hifadhi hizi zina muda mfupi tangu kaunzishwa, hivyo ni mwanzo mpya kwa jamii inayozizunguka kujifunza na kupata uelewa wa kutosha kuhusu Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na namna wanajamii wanavyoweza kuwa sehemu ya hifadhi hizi, ikiwa ni pamoja na kuzilinda na kunufaika nazo.

Hifadhi za Taifa kupitia kitengo cha Mahusiano ya Jamii wamekua wakitoa elimu ya uhifadhi kwa jamii ili kujenga uelewa wao kuhusu Hifadhi za Taifa na uhifadhi kwa jumla.

Katika utekelezaji wa jukumu la utoaji wa elimu ya Uhifadhi, wanajamii wawili wamekuwa mfano wa kuigwa miongoni mwa wananchi wanaozunguka Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe. Wanajamii hawa wamekuwa sehemu ya utoaji elimu ya uhifadhi kwa kuelimisha wanajamii wenzao kuhusu Hifadhi hizi kwa namna ambayo inasaidia jamii kujenga uelewa na kushiriki katika fursa pana ya utalii wa Hifadhi za Taifa.

Mzee Peter Daniel Lyakingilwe (77), maarufu kama 'Mzee Hururu' ni Sajenti Mstaafu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na veterani wa Vita ya Kagera. Pamoja na uanajeshi wake, udereva na ufundi makenika, Mzee Hururu ni msanii maarufu wa

mashairi, akitamba katika wilaya za Kyerwa na Karagwe.  Anatumia kipaji chake kutunga mashairi kuhusu Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe.

Aliimba moja ya mashairi yake katika warsha ya kuhamasisha utalii wa ndani iliyoandaliwa na wadau wa uhifadhi na maendeleo wanaofahamika kwa jina la 'Tanzania Nuru ya Amani'. Shairi lake lilijikita katika kuonesha faida za uhifadhi kwa jamii na kuhamasisha kushiriki kulinda maliasili, fursa za kiuchumi zinazoletwa na Hifadhi kwa jamii.

Mwishowe, ilikuwa kuhamasisha jamii kutembelea Hifadhi za Taifa ili kupata mapumziko na kuchangia uchumi wa nchi. Baadhi ya mashairi ya Mzee Peter Hururu ni kama ifuatavyo;-

'Wananchi hamasika, tukajali utalii.
Watanzania inuka, mbuga zetu tutalii.
Watanzania stuka, nchi yetu kubadili.
Ibanda Wilaya Kyerwa, Twaomba mtupokee'

'Ndugu zetu tunaomba, mapori yetu tulinde. Hata wanyama twaomba, Watanzania tulinde. Fisi chui hata simba, twiga tembo tuwalinde. Ibanda Wilaya Kyerwa, Twaomba mtupokee'.

Mzee Hururu anasema kwamba baada ya maofisa hifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kuona kipaji chake, walimkaribisha kwa ajili ya kutumia Sanaa hiyo kuuhamaisha umma juu ya uhifadhi na utalii, na alibahatika kwenda kwenye uzinduzi wa Hifadhi ya Ibanda-Kyerwa mkoani Geita.

Lakini pia aliimba mashairi huko Kayanga, ambapo alirekodiwa na kurushwa na Radio Badeko na Radio Karagwe na sasa anajiandaa kutunga mashairi mengine akishapata miongozo juu ya mada anuai.

Kwa umri wake ameona mengi na anasema kwamba zamani mwamko wa Watanzania kwenye uhifadhi haukuwa mkubwa, tofauti na sasa ambapo watu wengi, ikiwa ni pamoja na watoto wadogo na walio shuleni wanazungumzia uhifadhi na utalii na wanaelewa vyema.

"Hifadhi zilipoanzishwa zamani mwamko haukuwa mkubwa japo viongozi walidhamiria hivyo. Sasa mambo ni makubwa na tofauti sana, yamebadilika. Kuja kwa hifadhi hizi mbili huku kwetu kunaibua ari mpya ya utalii na kuamsha upendaji wa uhifadhi kwa faida ya kizazi cha sasa na vijavyo," anasema Mzee Hururu aliyesoma hadi darasa la nne la Mkoloni na kuwa Kiongozi wa TANU Youth League wa Kata ya Nyaishozi.

Ameweka historia kubwa kwa kuimba kwaya kanisani, lakini pia kuongoza vijana kuimba nyimbo za wakati wa Uhuru wa Tanganyika 1961. Anajivunia uzalendo wake, kwani anayo Shahada ya Upiganaji kutokana na kushiriki Vita ya Kagera.

Mwingine ni Mzee Martin Ruta maarufu kama 'Mzee Mashuhuri', huyu ni Mwenyekeiti wa Wazee wa Wilaya ya Kyerwa na ni mkazi wa Kijiji cha Kibingo, wilayani Kyerwa. Mzee huyu amekuwa akitoa elimu ya uhifadhi kuhusu Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe katika vikao mbalimbali anavyoshiriki.

Amekuwa akifanya hivyo kuanzia ngazi ya kijiji hadi kwenye Baraza la Madiwani la Wilaya ya Kyerwa. Licha ya umri wake, mzee huyu amekuwa na uelewa mpana kuhusu fursa zinazoletwa na Hifadhi za Taifa na kuhamasisha jamii yake kushiriki katika kuhifadhi na kuchangamkia fursa za uwekezaji katika biashara ya utalii.

Mzee Mashuhuri huwa pia mstari wa mbele katika kutoa taarifa za historia za Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe tangu zikiwa mapori tengefu na Mapori ya Akiba. Taarifa hizo ni muhimu katika mipango ya ustawi wa Hifadhi hizi mbili, haswa katika uboreshaji wa uhifadhi wa maliasili.

Wanajamii hawa, Mzee Hururu na Mzee Mashuhuri wanaonesha mfano kwa jamii yao katika kuona fursa ya uhifadhi na kushiriki katika kuelisha na kuhamasisha uhifadhi wa Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe.

Ni kawaida kwa jamii nyingi kwamba mabadiliko hupokelewa haraka na vijana lakini wazee hubakia na msimamo wa zamani. Lakini ni tofauti kwa wazee hawa; wamekuwa watu wa kwanza kupokea uanzishwaji wa hifadhi hizi na kuchukua hatua ya kusaidia katika kutoa elimu na Kuhamasisha jamii yao kuhusu uhifadhi. Wanajamii hawa, licha ya kuwa msaada kwa jamii, ni msaada mkubwa kwa hifadhi katika kufikisha elimu ya uhifadhi kwa jamii na kukuza mahuasiano kati ya Jamii na Hifadhi.

# HIFADHI SAADANI NA MSAADA WA ZAHANATI KWA WANAKIJIJI MKANGE

"Kwa sasa huduma zimeboreka sana kwa sababu ya uzuri wa miundombinu na hata wajawazito wanahamasika kuja kujifungua hapa" anasema Mugeta, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mkange.



Katika Halfa ya kukabidhi mradi kati ya wageni alioudhuria ni Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete; Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo; Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete na mkuu wa wilaya ya Chalinze na viongozi kutoka Halmashauri ya Chalinze.

Na Romanus Mkonda,

AFYA ni moja ya misingi na nguzo muhimu za maendeleo ya watu na jamii popote duniani, na afya haiwezi kuwa nzuri pasipo kuwa na huduma bora za afya katika miundombinu imara.

Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limekuwa mstari wa mbele kushirikiana na wanavijiji wanaopakana na hifadhi kwenye mambo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kusaidia kuweka na kuboresha miundombinu ya afya.

Hifadhi ya Taifa Saadani ni moja ya hizo, ikiwa inapatikana katika mkoa ya Pwani - wilayani Bagamoyo na Chalinze na katika Mkoa wa Tanga wilayani Pangani na Handeni.

Hifadhi hii ina ukubwa wa kilomita za mraba 1,100 baada ya kupandishwa hadhi lililokuwa Pori la Akiba Saadani. Ni eneo lililokuwa Ranchi ya Mifugo Mkwaja, Msitu wa Zaraninge na Mto Wami unapoingilia baharini. Hifadhi hii ilitangazwa rasmi mnamo mwaka 2005 kwa Tangazo la Serikali (GN) namba 281.

Hifadhi ya Taifa Saadani inazungukwa na vijiji 16. Maofisa wa Hifadhi ya Taifa Saadani wamekuwa wakiwafikia wananchi kwa kuwapa elimu juu ya uhifadhi na kuhamasisha wananchi washiriki katika ulinzi wa rasilimali za asili zilizopo ndani na nje ya Hifadhi.

Aidha, hifadhi imekuwa ikitekeleza sera ya wananchi kunufaika kwa uwapo wake katika

kushirikiana na wananchi katika utekelezaji wa miradi ya kijamii.

Katika Kijiji cha Mkange kilichoko Kata ya Mkange, Halmashauri ya Chalinze, Hifadhi kwa kushirikiana na jamii imetekeleza mradi wa zahanati uliogharimu fedha za Kitanzania 304,905,630/-. Utekelezaji wa mradi huu ulizingatia sera ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) inayotaka wananchi kuchangia asilimia 30 na Hifadhi kuchangia asilimia 70 kwenye mradi husika.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mkange, Prosper Mugeta, anasema kwamba lengo ni zahanati hiyo kupandishwa hadhi hadi kuwa Kituo cha Afya ikishakidhi vigezo na masharti na anawashukuru Hifadhi ya Taifa Saadani kwa msaada huo.

Anasema TANAPA wameshiriki tangu hatua za awali kabisa za ujenzi wa kituo hicho mwaka 2014, ambapo wananchi walichangia nguvu kazi, ikiwa ni pamoja na kusomba mawe, kokoto na maji. Anasema huduma awali zilikuwa hafifu kutokana na kukosa kituo bora chenye miundombinu stahiki, lakini sasa wanajivunia kuwa moja ya kata zenye vituo bora vya afya.

"Kwa sasa huduma zimeboreka sana kwa sababu ya uzuri wa miundombinu na hata wajawazito wanahamasika kuja kujifungua hapa kwa sababu hupumzishwa kwa muda hadi wanapokuwa na uwezo wa kurudi makwao, kukiwa na samani nzuri na huduma bora kutoka kwa mganga anayeishi mahali pazuri na mwenye hamasa ya kazi," anasema Mugeta.

Kituo hiki kinatoa huduma kwa vijiji vitano vya Mkange, Mandamazingara, Gongo, Matipwili na Saadani.

Wakati wa utekelezaji wa mradi huu, mara nyingi imekwa vigumu jamii kukamilisha 30% zinazohitajika na kufanya Hifadhi kutoa



gharama kubwa zaidi ya 70%. Katika mradi huu jamii waliweza kuchangia kiasi cha 70,194,689/- na TANAPA kupitia Hifadhi ya Taifa Saadani walichangia 234,710,941/-. Katika mradi huu lilipatikana Jengo la Wagonjwa (OPD), nyumba ya daktari, choo, kasha moto (incinerator), tenki la kuhifadhia maji na samani za zahanati.

Mradi huu ulikabidhiwa kwa jamii mnamo Februari 2020 ili utumike kwa jamii. Katika Hafla ya kukabidhi wa mradi kati ya wageni walioudhuria ni Pamoja na Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete; Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo; Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete na mkuu wa wilaya ya Chalinze pamoja na viongozi wengine kutoka Halmashauri ya Chalinze.

Kutokana na mradi huu, hamasa kwa jamii katika kushiriki kwenye shughuli za ulinzi wa rasilimali za asili na kufichua wahalifu imeongezeka. Mwanzoni Kijijij cha Mkange kilikuwa na wahalifu wengi wa wanyamapori na ukataji magogo hifadhini.

Aidha, mradi huu unawahakikishia jamii kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya karibu na makazi yao badala ya kwenda mbali. Kwa hakika, wameona na kutambua mchango halisi wa Hifadhi ya Taifa Saadani katika maisha yao ya kila siku.

Mganga Mfawidhi wa Mkange, Dr Musa Sambo anasema kwamba awali jengo halikuwa bora na hivyo pia huduma kuwa hafifu tofauti na sasa ambapo wapo vyema kutokana na msaada wa TANAPA kupitia Hifadhi ya Taifa Saadani.

"Leo hii hata ari ya kuchapa kazi imepanda kwa sababu tupo kwenye jengo zuri, nyumba nzuri kwa daktarin na watumishi – hali inaridhisha kwa hakika na ni jambo la wazi kwamba ili utoe huduma bora ni muhimu kuwa katika mazingira mazuri. Wametupa samani pia; awali viti vilikuwa vibovu hata unaweza kufa ganzi. Wajawazito wanakuja kwa mahudhurio mazuri kujifungua," anasema.

Anaongeza kwamba hata jitihada za kuzuia maambukizi zimeboreshwa kwa sababu ya kupata kashamoto (incinerator) kwa ajili ya kuteketeza taka, wamepata rafu (shelf) kuhifadhi vitu. Anaishukuru TANAPA kwa kuwapa mazingira mazuri kituoni hapo na anawaasa wateja wake na wananchi kwa ujumla kudumu katika uhifadhi wa mazingira, kuwalinda Wanyama na hifadhi kwa sababu ni kwa kustawi hifadhi wataweza tena kupata misaada kama huo mkubwa.

Mmoja wa wanavijiji, Msekeni Juma Ramadhani (46) anathibitisha kwamba sasa huduma zimeboreshwa, zikitolewa kwa muda na wanapata dawa kwa wakati mwafaka, daktarin anaishi, kulala pazuri na ofisi nzuri, vyoo vipo na maji safi na salama yanapatikana bila shida. Hiyo ndiyo raha ya wananchi kuwa karibu na Hifadhi ya Taifa Saadani.

# JITIHADA ZA KUNUSURU USHOROBA NA MFUMO WA IKOLOJIA GOMBE ZAANZA KUZAA MATUNDA:




## Matukio ya moto yamepungua.

***Na Nelson Mcharo***

Hifadhi ya Taifa ya Gombe iko katika Mkoa wa Kigoma, Wilaya ya Kigoma Vijijni, kandokando ya Ziwa Tanganyika, umbali wa kilomita 16 kaskazini mwa mji wa Kigoma ambao ni makao makuu ya mkoa.

Hifadhi hii ni miongoni mwa Hifadhi 22 zinazosimamiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA). Hifadhi ilitangazwa rasmi kuwa hifadhi ya Taifa mwaka 1968, ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 35 zikijumuisha milima na mabonde. Mnamo Julai 2013 Serikali kupitia tangazo la gazeti la serikali namba 228 liliongeza eneo la Ziwa Tanganyika lenye ukubwa wa kilomita za mraba 21.2 katika eneo la hifadhi ya Taifa Gombe, hivyo kufanya eneo la Hifadhi kuongezeka hadi kufikia kilomita za maraba 56. 2. Hifadhi hii ni makazi ya wanyama adimu sana duniani aina ya Sokwe mtu, wanyama ambao pia wako hatarini kutoweka katika uso wa Dunia.

Katika mfumo wa kiikolojia, Hifadhi hii ni kitovu cha mfumo mkubwa wa kiikolojia unaoanzia Gombe hadi Masito Ugala na Gombe-Burundi (Mkamba Hill). Mfumo huu wa kiikolojia unawezeshwa kwa kuwa na shoroba mbili ambazo ni Gombe-Kwitanga ambapo Sokwe walikuwa wanatumia ushoroba huu kwenda Kwitanga na mwingine ni Gombe-Mukungu-Rukamabasi ambao unatumiwa na Sokwe kutoka Hifadhi ya Taifa ya Gombe kwenda mpaka Burundi.

Ushoroba wa Gombe-Mukungu-Rukamabasi.

Ushoroba ni sehemu au kipande cha ardhi kinacho unganisha maeneo mawili au zaidi ambapo wanyama pori hutumia kama njia au mapito yao wanapohama. Wanyamapori hutumia ushoroba kutoka eneo moja kwenda eneo jingine kwa ajili ya kutafuta mahitaji yao muhimu kama vile chakula, mazalia, kulelea Watoto, kukwepa majanga ya asili na kukwepa hali ya hewa mbaya katika eneo moja. Maeneo hayo yanaweza kuwa yamehifadhiwa au hayajahifadhiwa kisheria. Maeneo hayo yanaweza kuwa mapori ya akiba, mbuga za wanyama za Taifa na Hifadhi za Misitu.

Gombe-Mukungu-Rukamabasi ni ushoroba unaotumiawa na Sokwe wanapohama kutoka Hifadhi ya Taifa Gombe kwenda kaskazini mwa hifadhi hadi mpakani mwa nchi ya Tanzania (Kagunga) na Burundi na hatimaye kuingia Burundi. Ushoroba

huu unaanzia kusini mashariki katika kijiji cha Kigalye kusini na kuelekea kasikazini mashariki mwa Hifadhi ya Taifa ya Gombe.

Kuanzia mwaka 1998 hadi 2005, shughuli za kibinadamu zilianza kuonekana katika ushoroba huu ambazo zilileta athari kubwa za kimazingira. Uharibifu mkubwa uliotokana na uvamizi wa misitu kwa ajili ya kufungua mashamba, kuvuna mbao, makazi na kuchoma mkaa ulisababisha kuharibu ushoroba huu na kuzuia Sokwe kuendelea kutumia kama mapito yao ya hapo awali.

Mwaka 1992 Idara ya Ujirani Mwema ilianzishwa katika Hifadhi ya Taifa Gombe. Idara pamoja na kazi zingine imejikita zaidi katika kutoa elimu ya uhifadhi na kuendelea kujenga na kuimarisha mahusiano kati ya Hifadhi na jamii zinazizunguka. Aidha Idara inashirikiana kwa pamoja na wadau wa uhifadhi kama "Root and Shoot" na "Lake Tanganyika Catchment Reforestation and Education" (TACARE) ambavyo vipo chini chini ya Taasisi ya Jane Goodall.

Kupitia ujilani mwema na wadau wa uhifadhi, juhudi mbalimbali za kunusuru Ushoroba huu zimefanyika kama ifuatavyo:-

Kupitia elimu ya Uhifadhi wananchi katika vijiji vinavyozunguka ushoroba huu na kupakana na hifadhi walielimishwa juu ya umuhimu wa ushoroba huu hivyo uharibifu ulipungua kwa kiwango kikubwa katika vijiji hivyo na kuunga juhudi za kupanda miti ya asili katika maeneo yaliyoharibiwa ili kuweza kurudisha msitu ulio kuwepo awali. Zoezi hili limefanikiwa kwa upande wa kusini na Mashariki mwa Hifadhi katika vijiji vya Mgaraganza, Kigalye, Mtanga, Mwamgongo na Chankele. Vijiji vya Mtanga na Kigalye ambavyo vilikuwa vinasumbuliwa na momonyoko wa udongo kwenye miaka ya 2000 na 2002 sasa imebakia historia.

Hashim Msaguzi (38) mkazi wa kijiji cha Bubango ni mmoja wa wanufaika wa jitihada za kunusuru ushoroba na ikolojia ya Gombe baada ya yeye na wanakijiji wenzake kushirikishwa katika mpango wa utoaji wa elimu ya mazingira na uhifadhi.



Picha ya Msitu wa kijiji cha Kigalye mwaka 2020

Msaguzi anakiri wazi kuwa baada ya kupata elimu hiyo,walianzisha kikundi cha watu 28 ambao walianzisha miradi ya ufugaji nyuki inayosaidia kuhifadhi mazingira ya ushoroba huo uliokuwa umeharibiwa na shughuli za kibinadamu.

"Matukio ya moto yaliyokuwa yameshamiri sasa yamepungua au kwisha kabisa.Tulikuwa na matukio ya moto kuanzia Julai, lakini baada ya kupata elimu ya utunzaji wa mazingira hakuna tukio lolote,na sote sisi ni walinzi wa mazingira yetu.

"Zamani nyani walikuwa adui wetu kwa sababu ya uharibifu wao kwa mazao yetu, lakini sasa hivi hakuna mwananchi anayethubutu kumuua nyani kwa sababu tumefundishwa mbinu za kuwadhibiti bila ya kuwadhuru na tumefanikiwa sana. Sasa tunaelewa umuhimu wa hawa wanyama kwa uhifadhi,"anasisitiza Msaguzi ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa kikundi cha Ushirika.

Kauli ya Msaguzi inaungwa mkono na Ramla Saidi (45),mkazi wa kijiji cha Chankele ambaye kupitia kikundi chao kinachoitwa PWITUNGE, chenye wanachama 18, wameanza kufaidi matunda ya uhifadhi.

Baada ya kupewa mizinga 20 ya ufugaji nyuki sasa waeanza kujikita katika uzalishaji asali ikiwa ni shughuli mbadala na wana matumaini ya kupata kipato cha



kutosha, hasa baada ya kupewa elimu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

"Awali sikujua thamani ya nyuki lakini baada ya kuelimishwa, tunajivua kuwa sehemu ya wahifadhi wa mazingira yanayopakana na Hifadhi ya Taifa ya Gombe, tunafanya doria mara mbili kila mwezi na kwa kweli tunategemea kufaidika na mengi,"anasisitiza Ramla

**Kutekeleza Mpango Matumizi Bora ya Ardhi.**

Mwaka 2008-2010 kupitia taasisi ya Jane Goodal iliwezesha mchakato wa kutengeneza mpango wa matumizi bora ya Ardhi katika vjiji vyote vinavyozunguka Ushoroba huu pamoja na vile vinavyopakana na Hifadhi ilikuweza kutenga eneo la ushoroba huo kuwa eneo la Hifadhi ya misitu ya Kijiji .Mpango huu umesaidia kwa kiwango kikubwa kwani wananchi waliweza kupanga matumizi ya Ardhi katika vijiji na waliokuwa wamevamia eneo la ushoraba huu kwa ajili ya makazi na kuanzisha mashamba walitoka na sasa msitu unaendelea kurudi katika hali yake ya awali.

**Kuazisha Miradi ya Ufugaji Nyuki**

Ili kuwafanya wananchi waweze kujipatia kipato cha kukidhi mahitaji yao bila kutegemea kupata mahitaji hayo kutoka kwenye msitu kwa kuvuna mbao, kuazisha mashamba na kuchoma mkaa. Vijiji vitatu vya Mgaranganza, Bubango na Chankele viinavyozunguka huu ushoroba vimewezeshwa mradi wa ufugaji nyuki kibiashara ndani ya eneo la msitu wa ushoroba kama mbadala wa kujipatia kipato bila kuharabu ushoroba na Hifadhi. Jumla ya mizinga 120 iligaiwa kwa vikundi katika vijiji tajwa hapo juu.



Mizinga ya Nyuki ikiwa imetundikwa katika eneo la ushoroba kijiji cha Mgaragaza

**Changamoto**

Pamoja na juhudi hizi bado kuna baadhi ya wananchi wanaendelea kuhujumu juhudi hizi kwa kuendelea kuharibu ushoroba kwa kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa, kupasua mbao na kufungua mashamba. Aidha uharibifu huu unachangiwa na sababu mbalimbali kama viongozi wa Kisiasa (Diwani, Wenyeviti wa kijiji) kushindwa kuwawajibisha wananchi wanaokiuka sheria za mpango wa matumizi bora ya Ardhi kwa kuhofia kukosa kura wakati wa uchaguzi, Wahamiaji haramu kutoka nchi jirani (Congo na Burundi), viongozi kushindwa kuwajibisha ndugu zao wanapo fanya uharibifu.

Uvunaji wa miti kwaajili ya kuchoma mkaa



**Tanuru la Mkaa ndani ya eneo la ushoroba**

# ULINZI SHIRIKISHI WAPUNGUZA UJANGILI WA SAMAKI RUBONDO

***Na David Kadomo,***

Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo ni moja kati ya Hifadhi za Taifa 22 hapa Tanzania. Kikiwa ni kisiwa cha pili kwa ukubwa katika Ziwa Viktoria, Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo inasifika kwa kuwa na bioanuai mbalimbali, wakiwamo wanyamapori wa asili (indigenous wildlife species) na wale waliopandikizwa (introduced wildlife species). Wanyama wa asili ni pamoja na swala aina aina ya Nzohe (Sitatunga), Pongo (bushback), Viboko, Tumbili (Velvet Monkeys) na Mamba. Wanyama waliopandikizwa ni pamoja na Sokwemtu, Twiga, Tembo, Mbega weupe na weusi na ndege aina ya Kasuku wa kijivu.

Pamoja na kuwa na vivutio vya wanyamapori na msitu wa kipekee, hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo ni mazalia ya samaki wa aina mbalimbali. Ukiachilia Hifadhi ya Kisiwa cha Saanane, Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo ndio eneo kubwa la mazalia ya samaki yaliyohifadhiwa vizuri ndani ya ziwa Viktoria. Samaki maarufu wanaopatikana ni pamoja na Sato (Tilapia) na Sangara (Nile perch).

Ujangili wa samaki ndio changamoto kubwa iliyokuwa inaikabili Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo. Hii ilitokana na ukweli kwamba wavuvi wanaoishi katika vijiji jirani na Hifadhi walikuwa wanamini kuwa wanapofanikiwa kuingia ndani ya hifadhi wangepata mapato makubwa kutokana na wingi wa samaki ndani ya eneo la hifadhi.

Kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 pekee, idadi ya majangili wa uvuvi waliokamatwa hifadhini walikuwa 631 katika matukio 742. Aidha zana za uvuvi zilizokamatwa hifadhini zilikuwa nyavu za kokoro 104, mitumbwi 700, nyavu aina ya timba (monofilament nets) 460 na nyavu za sangara 2,952.

Katika kukabiliana na changamoto hii ya ujangili, hifadhi kupitia idara ya mahusiano ya jamii, iliandaa mkakati maalumu wa kuelimisha jamii zinazopakana na hifadhi kuhusu mbinu bora za uvuvi endelevu na kuwahamasisha wananchi kutenga maeneo katika ardhi zao za vijiji vya mwambao wa Ziwa Viktoria yatakayohifadhiwa kama mazalia ya samaki.

Katika kutekeleza hili, wananchi walielekezwa kuacha kuharibu uoto ulioko kandokando ya ziwa, kwani ndani ya uoto huo ndipo samaki hutagia na kukuzia vifaranga. Maeneo ambayo yalipendekezwa na vijiji na kuonekana uoto wake umeharibiwa, Hifadhi kupitia Idara ya Ikolojia iliwaelimisha wananchi namna ya kurejesha uoto huo kwa kupanda mimea stahiki ili kuvutia samaki kuzaliana.

Zoezi hili limetekelezwa katika eneo la kijiji cha Nkome katika wilaya ya Geita, ambapo uoto wa ardhi oevu katika mwambao wa Ziwa Victoria umeweza kurejeshwa na kuvutia samaki kuzaliana.

Kupitia mpango huu, Hifadhi imeweza kuhamasisha vijiji vya Mwerani, Nyabugera, Kikumbaitale, Mlimani, Mkuyuni na Chato vyote vya wilaya ya Chato kuanzisha na kutenga maeneo ya mazalia ya samaki kwenye ardhi za vijiji vyao ndani ya Ziwa Viktoria.

Hifadhi kupitia mpango wa  Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) wa kuwezesha Miradi ya Ushirikiano wa Kijamii (SCIP) iliweza kuvipatia vijiji vya Mwerani na Nyabugera boti na injini kwa ajili ya kufanya doria kudhibiti ujangili, ili kulinda eneo lao la mazalia ya samaki. Doria za kudhibiti ujangili kwenye vijiji hivi zimekuwa zikifanywa na BMU (Beach Management Unit) ya vijiji hivi. Vijiji vya Mlimani, Mkuyuni na Chato vyote vya mjini Chato kupitia kikundi cha Gezaulole walipewa boti na injini kwa ajili ya kuwawezesha kufanya doria kwenye eneo lao la mazalia ya samaki.

Marco Nyahinga ni Mwenyekiti wa BMU ya Mwerani anayesema wanafanya kila wawezalo kuhakikisha ulinzi wa rasilimali na utunzaji mazingira kwa kutenga na kulinda mazalia ya samaki kwa kupiga doria.Nyahinga anasema wapo viongozi 10 wa BMU na kimsingi kila mvuvi halali anatakiwa kuwa mjumbe wa BMU husika, akiongeza kwamba hadi sasa wana wanachama 170.

"Kwa kweli tunajitahidi sana kwenye kazi hii ya kutenga maeneo na kulinda rasilimali na mazingira japokuwa kuna baadhi ya wavuvi wanajidai kuwa wajanja na hujiingiza katika uovu wa kuharibu mazalia na kuvua isivyotakiwa," anasema.

Anasema changamoto ni kwamba wanafanya kazi bila silaha, hivyo kulazimika wakati mwingine kujihami. Pamoja na hayo, pamekuwapo mafanikio makubwa ya udhibiti wa ujangili na vitendo haramu vya uvuvi hasa kwenye vijiji vilivyowezeshwa boti na injini kwa ajili ya kufanyia doria.

Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, BMU ya kijiji cha Mwerani, walifanikiwa kukamata jumla ya nyavu haramu aina ya timba 517, nyavu za kokoro tisa na nyavu haramu za sangara 30 vinavyokadiriwa kuwa na thamani ya 3,768,000/=. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 BMU hii ya kijiji cha Mwerani walifanikiwa kukamata nyavu haramu aina ya timba 110, nyavu za kokoro 25, vyavu haramu za sangara 26 na watuhumiwa 13 vyote vikikadiriwa kuwa na thamani ya 51,675,000/=.

Kikundi cha Utunzaji Mazalia ya Samaki cha Gezaulole kinaongozwa na Mwenyekiti James Lusanzu anayesema kwamba wana jumla ya wanachama 27, wanawake wakiwa 10. Kikundi hiki ni cha kipekee kwa sababu kinajumuisha pia watu wenye uhitaji maalumu kama bubu na viziwi.

Lengo lao ni uhifadhi na ndiyo maana wamewajumuisha watu tofauti ili wajue masuala ya uhifadhi na wamo madereva wa boti.

"Tulipewa semina na watu wa TAMAVITA tukaona umuhimu wa kuwachukua na tunao wanne wenye huo uhitaji maalumu. Waziri mwenye dhamana ya walemavu alikuja pia huku na tumeshirikiana kadhalika na walimu wa Shule ya Msingi Chato," anasema Lusanzu.

TANAPA chini ya Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo iliwapatia vifaa kama boti Aprili 2019 na kazi ikafanyika kwa manufaa makubwa kwa kikamata nyavu zenye thamani ya 38,125,300/- zilizokuwa zikitumiwa na wavuvi haramu.

Pamoja na kuendesha operesheni hizo dhidi ya ujangili, wameshirikiana na wananchi kwa kuwapa uelewa ili wajitambue na kutunza mazingira. Tayari mambo yameanza kuwa mazuri, kwani katika vijiji vinne vya jirani, ikiwa ni pamoja na Mlima Lubambangwe uwekezaji umefanyika na tayari wanajijengea zahanati pasipo kuwachangisha sana wananchi.

Kinachofanyika, anasema, ni kukodisha watu wa kuvua kwa nyakati maalumu na huwalipa kima cha kwenye 100,000/- kwa siku. Wameshafanya hivyo kwa awamu mbili hadi sasa wameingiza 11m/-.

Kikundi hiki kilikwenda katika Kijiji cha Murunba kufundisha, wakapunguza kwa kiasi kikubwa uvuvi haramu, uwekezaji ukafanywa na kijiji kuingiza 8m/- wakajenga ofisi nzuri ya kijiji na choo.

"Hiki sasa ni kijiji cha mfano kwa jinsi wananchi wanavyojiendesha na kusimamia uwekezaji, wakiwa wenyewe ndio wavuvi. Kijiji kingine ni Mbuge; hawa walitutaka tulinde kisha tuwe tunagawana kwa asilimia mavuno ya samaki au fedha. Kule wamesonga mbele, wanaongeza ujenzi wa madarasa na vyoo," anasema.

Pamoja na mafanikio ya kudhibiti vitendo haramu vya uvuvi ndani ya Ziwa Victoria iliyofanywa na vikundi hivi vya kiuhifadhi, kumekuwapo mwamko mkubwa sana wa kutunza mazalia ya samaki. Uhifadhi wa mazalia ya samaki umeimarika hasa kwenye maeneo hayo ya vijiji vilivyotenga maeneo ya Uhifadhi na samaki wameanza kuongezeka kwa idadi na ukubwa.

Hata hivyo, vikundi hivi vimekuwa vikikumbwa na changamoto mbalimbali, hasa ukosefu wa mitaji kwa ajili ya kununua mafuta ya kufanyia doria. Wajumbe wa BMU ambao ndio hufanya doria za mara kwa mara hukosa motisha, baadhi kujihusisha na vitendo vya ujangili kwa kushirikiana na wahalifu. Pia kuna upinzani kutoka kwa baadhi ya wavuvi haramu ambao wamekuwa wakijinufaisha na uvuvi haramu.



Pamoja na kuwa na vivutio vya wanyamapori na msitu wa kipekee, Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo ni mazalia ya samaki wa aina mbalimbali.

# ELIMU YA UHIFADHI, NA KUGAWANA FAIDA ZA UHIFADHI VYAPUNGUZA UJANGILI MIKUMI



Aliyekuwa Naibu waziri wizara ya Mali Asili na Utalii Mheshimiwa Costantine Kanyasu akipokea msaada wa mbegu bora za kilimo kwa niaba ya kijiji cha Muhenda kutoka kwa Balozi wa China hapa nchini Bi,Wang Ke.

## Mfuko wa SUKOS KOVA,China waunga mkono jitihada

***Na Lauthon A. Rwamulege,***

MUHENDA ni miong oni mwa vijiji 19 vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa Mikumi. Kinapatikana katika Kata ya Muhenda, Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro.

Kijiji hiki kina kaya 626 zenye jumla ya wakazi 3,079 ambapo wanaume ni 1,380 na wanawake 1,699 huku nguvu kazi ikiwa ni watu 709. Kijiji kina hati ya usajili No.MG/VC/54.

Kwa kipindi cha miaka mitatu, kuanzia 2015 hadi 2018 kijiji kilikuwa kinaongoza kwa takwimu za vitendo vya ujangili kwa wastani wa matukio 27 kwa mwaka.

Kutokana na hali hiyo kukithiri, Kitengo cha Mahusiano ya Jamii katika hifadhi hiyo kilifuatilia kwa karibu ili kubaini chanzo cha kukithiri kwa vitendo hivi vya ujangili.

Hilo lilifanyika kwa kufanya ziara za mara kwa mara katika kijiji hicho, kufanya mikutano na viongozi wa Halmashauri ya Kijiji, na pia mikutano ya hadhara ili kusikia moja kwa moja kutoka kwa wananchi na kutoa elimu ya uhifadhi.

Kitengo cha Mahusiano ya Jamii kiliona umuhimu wa kushirikisha makundi maalumu yakiwemo yale ya vijana, wanawake pamoja na wazee maarufu bila kuwasahau viongozi wa dini. Katika zoezi hili, kitengo cha Mahusiano ya Jamii kilibaini ukosefu wa shughuli maalumu ya kufanya hasa kwa vijana kutokana na baadhi kutojishirikisha na shughuli za kilimo na kuwaachia wazee na akina mama.

Pia ilionekana kuna umaskini wa kipato, hasa ukosefu wa vitendea kazi za kilimo ikiwa ni pamoja na ukosefu wa mbegu bora kwa ajili ya kilimo. Iligundulika kuwa baadhi ya wahamiaji katika kijiji hicho huandaa magenge ya vijana na kuwashawishi kushiriki katika vitendo vya ujangili.

Pia ilibainika kuwepo baadhi ya viongozi wa kijiji wasiokuwa waaminifu ambao walishindwa kukemea vitendo hivyo au kushiriki moja kwa moja katika



Kamishna Mwandamizi wa Uhifadhi kanda ya Mashariki Bi Asteria Ndaga akitoa neno wakati wa kukabidhi mbegu kijiji cha Muhenda.

vitendo hivyo.

Baada ya kubaini haya Hifadhi, kwa kushirikiana na Taasisi ya Suleiman Kova (SUKOS KOVA Foundation) pamoja na Ubalozi wa China nchini Tanzania, iliwapatia wana kijiji kiasi cha kilogramu 4,800 za mbegu mbalimbali za mazao ambayo ni choroko, alizeti na mahindi kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Meneja Uendeshaji wa Mfuko wa Sukos Kova, Rahma Kova anasema Mfuko huo ulitoa msaada kwa kushirikiana na Ubalozi wa China nchini baada ya kuona ujangili umeshamiri katika kijiji hicho.

"Tunaunga mkono jitihada za kupambana na ujangili, na njia bora tuliona na kuwapatia wakazi wa kijiji hicho njia mbadala ya kujipatia riziki kwa kuwapa mbegu zitakazowawezesha kulima mazao yatakayowapatia kipato.

"Tutaendelea kuwatafuta wafadhili wengine ili misaada ya namna hii ifike katika vijiji vingi zaidi zinavyozunguka Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ikiwa ni mchango watu katika kudhibiti ujangili na kulinda rasilimali za taifa ambazo zina manufaa makubwa kwa taifa letu,"anasisitiza Rahma na kuongeza:

" Tunatarajia kuandaa tathmini ya kazi hiyo, mafanikio katika mavuno na kuona jinsi ya kusonga mbele na wadau hao muhimu.

Anasema kwamba taasisi yao ilikuwa na malengo ya awali katika uhifadhi wa mazingira pamoja na kukabiliana na majanga, kutoa mafunzo kwa vijana kwenye maeneo hayo, lakini pia wamejiongoza katika masuala ya zimamoto na majini.

Hifadhi kupitia mpango wa kuwezesha miradi iliyoanzishwa na wananchi ilitoa mizinga 88 ya nyuki pamoja na vifaa vyake kwa kikundi cha ujasiriamali cha Mwangaza yenye

thamani ya sh 17,985,000.

Ilifanya hivyo kwa lengo la kuwawezesha kujipatia kipato kwa mtu mmoja mmoja kupitia kikundi chao. Kitengo pia kilifanikiwa kutoa mafunzo ya ujasiliamali kwa kikundi cha 'Umoja Tembo Pilipili' kwa kuwabadili kutoka mfumo wa VICOBA (Village Community Bank) na kuwaingiza katika mfumo COCOBA (Community Conservation Bank).

Mwenyekiti wa Kijiji cha Muhenda, Ndugu Franco anakiri kuwa tangu mwaka 2018 mpaka mwezi Agosti mwaka 2020 hakuna tukio lolote la ujangili lililotolewa taarifa kijijini hapo.

“Ni kweli vitendo vya Ujangili vimepungua sana hapa kijijini kwetu, tunawashukuru sana TANAPA kwa msaada na ushirikiano wao,'' anasema Franco.

Kutokana na mafanikio hayo, taarifa kutoka hifadhini zinaonyesha kwamba katika kipindi cha mwaka 2018/9 na 2019/20 hakukuwa na kesi ya ujangili kutoka katika Kijiji cha Muhenda.

Kiongozi wa askari wa hifadhi hiyo Zacharia Mwilasi anabainisha pia juu ya kupungua kwa vitendo vya ujangili katika kijiji hicho. Anasema kwamba kuna watu wanatumia njia za kijiji hicho kuingia hifadhini kwa nia ya kutenda uhalifu ila walipofuatilia uchunguzi ulionesha kuwa hawakuwa wakazi wa kijiji hicho.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Muhonda, Zinadu Masanza, anakiri kwamba kaya 926 zilifaidika kwa mbegu za mazao husika zilizotolewa na Hifadhi ya Taifa Mikumi na kwamba watu walivuna kwa namna tofauti kulingana na jinsi walivyootesha, kutunza na upatikanaji wa mvua.

Anakiri kuwa na ushirikiano mkubwa baina ya eneo lake na TANAPA pamoja na SUKOS KOVA Foundation, na kwamba tangu kuingia kwao kusaidiana, ujangili umepungua kwa asilimia kubwa sana.

“Tumepata usaidizi wa TANAPA na SUKOS KOVA Foundation, kwa asilimia kubwa kabisa ni kwamba ujangili umepungua kama si kuisha. Ni nadra sana kwa sasa kusikia suala la ujangili huku Mikumi,” anasema.

Kabla ya ushirikiano huo, anaongeza, vitendo vya ujangili vilikuwa vingi, ambapo nyamapori zilikuwa zikiuzwa maeneo mengi, lakini sasa ni ngumu kupatikana kwa sababu TANAPA na wananchi wanashirikiana kuwalinda wanyama, kuzuia uingiaji hifadhini na kuhakikisha mazingira yanalindwa.




Picha no 1.Makabidhiano ya mizinga ya nyuki na vifaa vyake kwa kikundi cha Mwangaza kijiji cha Muhenda.

# MRADI MKUBWA WA UFUGAJI NYUKI KUWA NEEMA KWA WAVIU



"Malengo makuu ya kikundi chao ni kuboresha afya ya wanachama, kuinua wigo wa mawasiliano na wadau wa afya na kutoa elimu ya kujikinga na virusi vya UKIMWI" anasema Kansila

Na Heriel Mollel,

ZIPO fursa nyingi katika jamii, hasa panapokuwapo ushirikiano baina ya mamlaka, taasisi, umma na watu binafsi, ambapo hata changamoto huweza kugeuzwa kuwa fursa.

Moja ya changamoto katika maisha ni magonjwa, kwani ukosefu wa afya ni msingi wa kushindwa kufanya kazi ngumu na kujipatia maendeleo. Hata hivyo, kwa mshikamano miongoni mwa wadau, makundi ya wenye changamoto hizo huweza kusaidiwa.

Moja ya makundi hayo ni Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU) ambao Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limewaangalia kwa jicho la tatu kuona jinsi ya kuwakwamua.

Baadhi ya hao ni wale wanaoishi katika Kijiji cha Kinyika, Kata ya Kinyika, Tarafa ya Matambo wilayani Makete katika Mkoa wa Njombe. Watu hawa wanaishi karibu na Hifadhi ya Taifa Kitulo. Hawa waliunda kikundi chao, kikiwa na wanachama 10 – wanawake tisa na mwanamume mmoja. Jordan Kansila ndiye mwenyekiti wa kikundi hiki kilichoanzishwa Mei 30, 2011



Mradi huu wa ufugaji nyuki ulizinduliwa na Mkuu wa Wilaya (DC) ya Makete, Veronica Kessy.

na kusajiliwa rasmi Oktoba 10, 2014 kwa kupewa hati ya usajili yenye namba MDC / CBO /041.

Kansila anasema kwamba miongoni mwa malengo makuu ya kikundi chao ni kuboresha afya ya wanachama, kuinua wigo wa mawasiliano na wadau wa afya na kutoa elimu ya kujikinga na virusi vya UKIMWI.

Wanalenga pia kujiendeleza kiuchumi kupitia zoezi la kukopa na kuweka na mradi wa nyuki na kutunza mazingira ya Chanzo cha Maji cha Igofi.

Juni 25, 2020 ilikuwa siku iliyojaa vifijo na nderemo pale Kikundi cha WAVIU kilipopokea Mradi wa Ufugaji Nyuki uliotolewa na TANAPA kupitia Hifadhi ya Taifa Kitulo.

Jumla ya mizinga 300 ya nyuki, vifaa vya kurinia asali kama vile mavazi maalumu, glovu, mashine ya moshi (gango la moshi), buti, nta na mashine ya kukamulia asali vyote vikiwa na thamani ya sh 17,575,000 vilikabidhiwa kwa WAVIU hao.

Mwenyekiti Kansila anasema kwamba mchango wa



*DC wa Makete, Veronica Kessy, akizindua mradi wa ufugaji nyuki kijiji cha Kinyika*

wanakikundi katika mradi huu ilikuwa ni nguvu kazi zao, ikiwa ni pamoja na kusafisha eneo la mradi, kukata milingoti, fito, nyasi za kuezekea banda la kufugia nyuki (apiary). Kazi ya utengezaji wa mizinga hii ilifanywa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Makete na kulipwa na Hifadhi ya inayozunguka Hifadhi ya Taifa Kitulo, kwani ufugaji wa nyuki una faida lukuki za kifedha kutokana na kuuza mazao ya nyuki.

Jingine ni kuongeza ushiriki wa jamii katika kutunza mazingira, kwa sababu ili nyuki wapate chavua ni lazima miti iwepo karibu. Kwa upande mwingine na uwepo wa Hifadhi yanonekanika.

"Ni matagemeo yetu kuwa mradi huu utachangia kipato kwa wanakikundi lakini pia utatunza chanzo cha maji cha Igofi na kuongeza mtiririko wa

maji katika mto Ruaha na hatimaye kwenye Mradi wa ufuaji wa umeme wa Bwawa la Nyerere (Stigler`s Gorge), lakini pia utasaidia wananchi kutambua thamani halisi ya maliasili na hivyo kuzilinda, ikiwa ni pamoja na kuongeza juhudi katika kuzitunza," anasema mwenyekiti huyo.



*Burudani zikiendelea wakati wa uzinduzi wa Mradi wa ufugaji nyuki kijiji cha Kinyika (Picha na Paschal Makumbule*

Taifa Kitulo. Mradi huu ulizinduliwa na Mkuu wa Wilaya (DC) ya Makete, Veronica Kessy.

Mradi huu unalenga kuondoa umasikini katika jamii

uwapo wa mradi huu utasaidia katika uchavushaji wa mazao ya chakula kwa jamii na pia kuongeza ushiriki wa jamii katika kutunza hifadhi kwani manufaa yatokanyo

Wananchi wanatakiwa kuhakikisha wanatokomeza vitendo vya kihalifu ndani ya hifadhi kama uwindaji haramu, uchimbaji wa chikanda, uvunaji wa miti na uchungaji wa mifugo ndani ya hifadhi.

Kansila anasema kwamba baada ya kuunda kikundi chao, wakaona kuna haja ya kutunza mazingira, kwa namna ya pekee kuhifadhi chanzo cha maji cha Igofi katika Mto Saloka kijijini Kinyika, na njia waliyoonelea

itakuwa nzuri ni kufuga nyuki hapo, kwani viumbe hao huwa askari wazuri katika uhifadhi wa mazingira.

Anasema kwamba nyuki waliingia kisha wakatoka lakini pia ilikuwa wakati dunia ikiwa imekumbwa na janga la virusi vya Corona, hivyo kwa sasa wanajipanga kuhakikisha wanashirikiana na maofisa

maliasili na maofisa nyuki kuhakikisha kwamba mradi huo unaenda kwa kasi inayotakiwa ili mafanikio yaje mapema.

Kansila anasema ipo changamoto ya watu kujiunga kwenye kikundi na wengine wanajitoa kwa sababu ya hofu ya kubaguliwa kutokana na hali yao. Mwenyekiti huyu ambaye pia hufanya ufuatiliaji wa hali za WAVIU na ufuasi wa dawa na maelekezo ya waganga, anasema wapo ambao huwafuata lakini wanamuuliza amejuaje hali zao, na hicho huwa moja ya vikwazo kwenye kazi yake hiyo ya kujitolea.

Ofisa Maendeleo ya Jamii (OCD) wa Kata ya Kinyika, Asifiwe Mwaitege anakiri kukijua kikundi hiki na kufanya nacho kazi kwa karibu.

"Licha ya kwamba ni WAVIU lakini wapo vizuri kiasi na wanajituma kwenye kazi lakini pia katika ufuasi wa dawa," anasema na kuongeza kwamba kwa taratibu, watu wasio WAVIU hawawezi kujiunga na kikundi kama hicho, kwani ni mahsusi kwa WAVIU hata kama wangetaka kuwaongezea nguvu.Mwaitege anasema kwamba mara yake ya mwisho kwenda kwenye mradi huu ni Desemba mwaka jana, na hiyo ni kutokana na umbali na changamoto ya usafiri, kwani kwa pikipiki ni sh 7,000 ambapo halmashauri ya wilaya haina utaratibu wa kugharimia usafiri.

Kamishna wa Uhifadhi wa Hifadhi ya Taifa Kitulo, Dora Batiho, anasema kwamba wanalenga kutoa semina tena kwa wahusika, ili kuhakikisha kwamba wanapata uelewa mpana juu ya dhana nzima ya ufugaji nyuki hadi hatua za kurina na kupata masoko ili kukuza uchumi wao wakati wakihifadhi pia mazingira

# USHIRIKISHWAJI WANANCHI WAMALIZA MIGOGORO YA MIPAKA MIKUMI



Pamoja na kuwa na vivutio vya wanyamapori na msitu wa kipekee, hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo ni mazalia ya samaki wa aina mbalimbali.

***Na Zawadi Mahinda***

HIFADHI ya Taifa Mikumi ilianzishwa mwaka 1964 kwa **Tangazo la Serikali Na 465**, ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 1,070. Mwaka 1975 Serikali iliongeza eneo upande wa kusini mwa Hifadhi na kufikia kilometa za mraba 3,230 kwa **Tangazo la Serikali Na. 121.** Hifadhi ipo katika mkoa wa Morogoro katika Wilaya za Kilosa, Mvomero na Morogoro Vijijini na inazungukwa na vijiji kumi na tisa (19) vilivyopo katika wilaya zote tatu na pia inapakana na Pori la Akiba Selous (kwa sasa Hifadhi ya Taifa Nyerere) kwa upande wa Kusini.

Hifadhi ya Taifa Mikumi ni miongoni mwa Hifadhi za Taifa ambayo kwa muda mrefu eneo kubwa halikuwa na alama za kudumu, hali iliyosababisha migogoro ya mipaka kati ya Hifadhi na vijiji. Hifadhi pia ilikuwa na migogoro ya muda

mrefu ya mpaka kutokana na baadhi ya maeneo ya vijiji kujumuishwa katika eneo la Hifadhi kutokana na makosa ya kutafsiri Tangazo la Serikali la Mwaka 1975 namba 121.

Mwaka 2017, Waziri Mkuu Majaliwa K. Majaliwa ilitoa agizo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha maeneo yote yaliyohifadhiwa yanawekwa alama za kudumu (Beacons) katika mipaka yake kwa kushirikisha wananchi ili kupunguza migogoro na Wananchi. Kutokana na agizo hilo la Serikali, Uongozi wa Hifadhi uliunda kamati ya mpaka iliyojumuisha Idara za Ulinzi, Ujirani Mwema na Ikolojia. Kamati hiyo kwa kutumia dhana ya Ujirani Mwema iliona njia pekee ya kumaliza migogoro hiyo ni kuhakikisha wananchi na viongozi wa Wilaya wanashiriki kikamilifu katika kila hatua ya zoezi la uwekaji wa alama za kudumu katika maeneo yote yenye migogoro na yasiyokuwa na alama za kudumu.

Vijiji ambavyo wananchi walishirikishwa katika zoezi hilo ni Maharaka, Doma, Mkata, Tindiga, Kilangali, Kiduhi, Mbamba, Mhenda, Kitunduweta, Ihombwe, Kisaki, Gomero na Nyarutanga pamoja na wataalam wa wilaya za Kilosa,



Mvomero na Morogoro Vijijini.

Hatua za ushirikishwaji zilivyofanyika

- Ofisi za Wakurugenzi watendaji na Wakuu wa wilaya za Kilosa, Mvomero na Morogoro vijijini pamoja na vijiji husika walijulishwa kwa barua juu ya zoezi la uwekaji wa vigingi katika maeneo ya Hifadhi yanayopakana na vijiji
- Vikao vya viongozi wa vijiji husika vilifanyika ambapo walielimishwa kuwa zoezi la uwekaji wa alama haliendi kubadili mipaka iliyopo kwenye Tangazo la Serikali lililotangaza Hifadhi ya Taifa Mikumi. Pia walipata nafasi ya kuteua wajumbe wanne hadi sita kushiriki kutambua maeneo ambayo Hifadhi itaweka vigingi

Ushirikishwaji wa wananchi kuhusu zoezi la uwekaji vigingi – Kijiji cha Kilangali

- Wataalam wa Wilaya (Afisa Maliasili, Mipango miji na wapima wa wilaya) walishiriki wakati wa zoezi la kufanya utatuzi wa migogoro ya mpaka kwa kuhakikisha kila mmoja Hifadhi na kijiji wanaweka alama zao katika mipaka yao sahihi inayotokana na Tangazo la Serikali na ramani za vijiji. Pia walishiriki kikamilifu kutambua maeneo ambayo vigingi vitawekwa

Kamati ya mpaka ya Hifadhi na Wataalam wa (W) Kilosa katika zoezi la uwekaji wa vigingi

- Kamati ya Ulinzi ya wilaya ya Kilosa pamoja na wataalam wa wilaya walishirikishwa kikamilifu kutatua baadhi ya migogoro katika vijiji vya Maharaka, Kilangali, Kitunduweta Kihelezo na Kitete Msindazi kabla ya zoezi la kuweka vigingi
- Wapima wa wilaya na wajumbe wanne hadi nane kutoka kila kijiji walishirikishwa wakati wa kutambua maeneo ya jira (coordinates) ambamo vigingi vimewekwa
- Wananchi walishiriki kusaidia upelekaji wa vifaa vya ujenzi katika maeneo ambayo alama za kudumu zinawekwa

Ni dhahiri Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ( MINAPA) ya sasa sio ya zamani kwani migogoro mingi ya mipaka iliyokuwepo tangu mwaka 2004 imeisha na alama za kudumu zimewekwa katika mpaka wa Hifadhi. Wananchi walishirikishwa vema na waliridhia alama hizo kwa kusaini katika fomu maalum za

makubaliano. Hivyo ushirikishwaji wa wananchi, viongozi wa Halmashauri zinazopakana na Hifadhi pamoja na wataalam wa ardhi wenye dhamana katika utatuzi wa migogoro ya mipaka ni njia sahihi ya kumaliza migogoro kuliko kutumia Wahifadhi na wataalam pekee.

Kamati ya mpaka na wataalam wakati wa usimikaji vigingi

Ushirikishwaji wa wananchi katika utambuzi wa maeneo ya kuweka beacon – Kijiji cha Kilangali Ushirikishwaji wa wananchi katika utambuzi wa maeneo ya kuweka beacon – Kijiji cha Maharaka Usimikaji vigingi kijiji cha Maharaka kwa kushirikiana na wawakilishi wa wananchi.

## BURIANI MHIFADHI MALIMA ERNEST MBIJIMA



Kwa huzuni na majonzi makubwa mioyoni mwetu, tunaandika wasifu wa Mhifadhi Malima Ernest Mbijima, mtumishi wa muda mrefu katika Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) katika Kitengo cha Mahusiano ya Jamii ambaye ametangulia mbele za haki.

Malima amefumba macho yake na kwa upole amemaliza safari ya maisha yake hapa duniani. Ameitwa na mola wake, kwa unyenyekevu ameitika. Ametuacha! Maisha yetu kwa sasa ni ya upweke na yasiyo na msaada wa Malima ambaye alikuwa mshirika wetu na tegemeo kubwa.

Mhifadhi Malima Mbijima alifanya kazi ya kutukuka kwa miaka 26, tangu alipoajiriwa Februari 16, 1995 katika Hifadhi ya Taifa Gombe na baadaye kufanya kazi katika hifadhi mbalimbali nchini hadi alipoitikia wito wa mola wake Julai 31, 2021 akiwa mjini Songea. Katika uhai wake, Malima alifanya kazi mbalimbali ndani ya Shirika, hususani katika Kitengo cha Ujirani Mwema na Mahusiano ya Jamii katika hifadhi za Arusha, Ruaha, Kitulo, Mkomazi, mradi wa SPANEST, Makao Makuu na mradi wa REGROW.

Mwanafalsafa maarufu aitwaye Albert Einstein aliwahi kusema, "Thamani ya binadamu huonekana kwa yale aliyoyatoa kwa binadamu wenzake na siyo aliyopokea." Mhifadhi Malima ni mfano dhahiri wa uthibitisho wa kauli hiyo. Kwa maneno mengine alifanya kazi kwa kujitoa, kwa ushirikiano na kwa bidii na maarifa yake yote. Aliishi kwa vitendo vilivyoacha alama itakayodumu kwa muda mrefu. Ndiyo maana leo tunaandika wasifu huu na kumbukizi ya kumuenzi kupitia ukurasa huu.

Tunakumbuka juu ya maisha ya Malima yaliyojaa ubinadamu, utu, heshima, upendo na uchapakazi usio wa mfano. Alikuwa na ujasiri na umakini wa kipekee, mfano bora wa mtumishi aliye msikivu, mwaminifu na mshauri wa kweli. Nje ya uhifadhi, alifahamika sana kama 'Mwalimu Malima,' 'Mchungaji Malima' kutokana na uhodari wake katika kufundisha na kulitetea neno la Mungu. aliwavuta wengi na kuwafundisha kazi, akihubiri na kufundisha habari za neno la Mungu huku akiwaombea.

Watumishi wa Kitengo cha Mahusiano ya Jamii kwa umoja wao wana mengi ya kumuelezea na kumuenzi Mhifadhi Malima kutokana na maisha yake katika utumishi, mchango katika jamii kama kielelezo cha mtu wa mfano kwa alivyojitoa na pia kumuenzi mwenyezi Mungu, vilevile alikuwa na mchango mkubwa sana katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku katika Kitengo cha Mahusiano ya Jamii kutokana na uelewa, uzoefu na kujituma kwake.

"Alinipa ushirikiano, ushauri usio na mashaka, aliniheshimu na kunipenda mimi na hata familia yangu, zaidi ya yote alikuwa ananiombea kwa Mungu. Hakika ni pengo kubwa sana kwangu kumpoteza msaidizi wa karibu, ni pengo kubwa kwa Wahifadhi wa Mahusiano ya Jamii na Shirika kwa ujumla," anasema Godwell Ole Meing'ataki Mkuu wa Kitengo cha Uhifadhi -TANAPA

"Kwangu Mhifadhi Malima alikuwa kama kaka, rafiki, ndugu, mwalimu na kimbilio. Alinifundisha kwa matendo na hakupenda kuongea sana. Nilitamani sana niwe kama yeye ila nilishindwa. Ameondoka wakati ameanza kunifundisha kumjua Mungu na kusimamia Imani," anaeleza Edmund Murashani aliyefanya kazi na marehemu katika mradi wa SPANEST.

Naye Heriel Masaki, Mhifadhi Mahusiano ya Jamii kutoka Tarangire anasema: "Mhifadhi Malima alikuwa mtu wa hekima na kadri muda ulivyoenda hekima yake iliongezeka hadi kuitwa mtumishi. Nilimfahamu kuanzia chuoni Mweka hadi anatutoka. Ushirikiano wake kwa watu ulikuwa jadi kwake. Tulishauriana naye kwa mengi ya kikazi na hata ya kijamii kabla ya kushauriana na wengine. Hakika Malima alifanya mengi kwetu". Marehemu Malima ameacha Mjane Nowadia Ntimi na Watoto watatu; Sechelela Malima (10), Witumbilo Malima (9) na Wendo Malima (2.5).


Buriani Malima, Tutakukumbuka Daima


# HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA

## KITENGO CHA UHIFADHI MAHUSIANO YA JAMII









**Mawasiliano:**
Kamishna wa Uhifadhi,
Hifadhi za Taifa Tanzania, S. L. P 3134, Arusha, Tanzania.
Simu: +255 27 250 297 0404/297 0405
Baruapepe: cc@tanzaniaparks.go.tz Tovuti: www.tanzaniaparks.go.tz
Twitter: @tzparks Instagram: tanzaniaparks Facebook: @tzparks